**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YAWAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule; 0752207442**

**Makamu Mkuu wa Shule;0765332992/075674118**

**Patron:0754218085**

**Shule ya Sekondari KIBENGU**

**S.L.P 360**

**MAFINGA**

**Iringa**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**

**……………………………………………..**

**S.L.P ……………………………………..**

**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBENGU HALMASHAURI YA WILAYA MUFINDI MKOA WA IRINGA MWAKA ……..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika Shule hii mwaka ……. na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Kibengu ipo umbali wa Kilometa 64 kaskazini mwa mji wa Mafinga. Namba ya mitihani ya shule ni S0659. Shule ni ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana kwa kidato cha kwanza hadi cha nne, na ni ya wavulana tu kwa kidato cha tano na sita. Tahasusi zilizopo ni HGL na HKL. Usafiri wa basi kutoka mji wa Mafinga unapatikana katika kituo cha mabasi Mafinga Nauli ni Shilingi 8,000 kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……………

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni suti ya koti mikono mirefu rangi ya blue nyeusi (dark blue). Suruali zishonwe vizuri, ziwe na marinda mawili na zisiwe nyembamba chini (pima inchi 16-18), ziwe na turn up na zivaliwe kiunoni kwa mkanda mweusi wa ngozi.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu yenye mfuko mmoja upande wa kushoto.
iii. Tai rangi ya blue nyeusi (dark blue).
iv. Sare ya Michezo ni bukta ya blue na T-shirt ya blue
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba visivyo na urembo
vi. Soksi jozi mbili nyeusi;
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta la shule rangi ya blue nyeusi(dark blue) lenye v kifuani
ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali mbili rangi nyeusi.
x. Tisheti (T-shirt) mbili aina ya form six rangi ya kijivu
NB. Hairuhusiwi kuja na nguo nyingine yoyote isiyo sare ya shule.
xi. Track suit moja rangi ya light blue
xii. Pullneck nyeusi mbili
xiii. Blanketi zito 1

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari counterbook kumi na mbili quire 4
ii. **Ream (A4, A one)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka; moja muhula wa kwanza na nyingine mhula wa pili.

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*) unaweza kumnunulia mwanao kama uchumi unaruhusu;
iv. Godoro la futi mbili na nusu lenye unene wa inchi 4.
v. Mashuka Jozi 2, moja rangi ya pink na jingine rangi blue bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1*;*
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (Sahani ya bati yenye vyumba, bakuli, kijiko na kikombe cha bati);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Vifaa vya Usafi
HGL- Kwanja, fagio ngumu, jembe na mfagio aina ya chelewa.
HKL - Kwanja, fagio laini (soft bloom), mopper aina ya squizer, jembe.
x. SCIENTIFIC CALCULATOR –{f(x) 991}
xi. Kamusi (dictionary) ya kiingereza kwa kiingereza
xii. Mafaili mawili (spring files) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi.
xiii. Tochi au taa ya sola kwa dharula umeme ukikatika
xiv. Sanduku la chuma linalofunga vizuri kwa kufuli kwa ajili ya kuhifadhia nguo zako.
xv. Cheti cha matokeo kidato cha nne.(Result slip).
xvi. Kadi ya bima ya Afya
xvii. Sabuni ya chooni lita 5
xviii. Jacketi jeusi la dukani Lisilokuwa na maandishi yoyote. (litavaliwa waakati wa baridi kali na usiku wakati wa kujisomea).
xix. Begi la kubebea madaftari “School Bag” rangi Nyeusi
xx. Kandambili aina ya umoja

## 2.3 Michango mbalimbali Shule ya Bweni

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hiyo 80,000 iingizwe kwenye akaunt na.60201200075, jina la akaunt, KIBENGU SECONDARY SCHOOL, BENK YA NMB tawi lolote au kwa wakala wa benki ya NMB. Wasilisha risit ya kulipia benk (bank pay in slip) kwa mhasibu wa shule pindi ufikapo shuleni. Tafadhali unapolipa andika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya benk.

## 3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xvi. Kudharau bendera ya taifa
xvii. Kufanyya jaribio lolote la kujiua
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
xix. Kuchelewa kuripoti shuleni baada ya likizo

**UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule namba 0752207442**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0765332992/0756741188**
- **Mwandamizi Taaluma 0756881433**
- **Mwandamizi malezi 0765752714**

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

**A. MWANAFUNZI NA WAZAZI/WALEZI WAKE**

i. Jina la mwanafunzi..........................................................................................................
ii.Tarehe ya kuzaliwa....................................mahali..........................................................
iii.Jina la baba..............................................yu hai/amefariki.............................................
iv. Mahali anakoishi;
Kijiji/Mji..............................kata............................tarafa............................................
v. Kazi ya baba...................................................................................................................
vi. Anwani yake..........................................................simu..........................................
vii. Jina la mama........................................yu hai/amefariki...............................................
viii. Mahali anakoishi;
Kijiji/Mji............................kata.............................tarafa............................................
ix. Kazi ya mama..................................................................................................................
x. Anwani yake.................................................................simu.......................................
xi. Jina la mlezi.....................................................................................................................
xii. Mahali anakoishi;
Kijiji/Mji.............................kata...........................tarafa.............................................
xiii. Anwani yake..........................................................simu..........................................

**B. NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI**

| NA | JINA | UHUSIANO | NA.YA SIMU/ANWANI |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |

**C. AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE(MWANAFUNZI)**

Mimi .................................................. naahidi kufuata sheria,kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakaokuwa ndani na nje ya shule.Sitajihusisha na migomo,fujo wala makosa ya jinai.

Sahihi.........................................tarehe...............................................

**D. AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ...................................................... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu,naahidi kumpatia ada ya shule,michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.

Sahihi........................................tarehe...................................................

**VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO/MAAGIZO HAYO HAPO JUU NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU.**

**...............................**
**JOHN JOHN MUTUGUMONGA**
**MKUU WA SHULE**

**PRIME MINISTER'S OFFICE-REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MUFINDI DISTRICT COUNCIL**
**KIBENGU SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognize Hospital in respect of all new entrants to Kibengu Secondary School.

Full name..........................................................................................................Age.........

1. Blood comment (Red &White) .......................................................................................
2. Urine examination........................................................................................................
3. Stool examination.............................................................................................................
4. Syphilis test.....................................................................................................................
5. T.B test...........................................................................................................................
6. Ear test..........................................................................................................................
7. Eye test..........................................................................................................................
8. Speen.............................................................................................................................
9. Abdominal.......................................................................................................................
10. Additional information or any other physical, hereditary or infectious disease:
    ..........................................................................................................................
    ..........................................................................................................................
    Treatment after examination:

..............................................................................................................................

**<u>MEDICAL CERTIFICATE</u>**

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education.
Signature.......................................................
Designation..................................................
Station........................................
Date.................................................. (official stamp) ................................

NB:Fomu hii ijazwe na Mganga katika hospitali inayotambulika na Serikali.

**KIBENGU SECONDARY SCHOOL**

**ESSENTIAL REFERENCE BOOKS/TEXT BOOKS FOR A-LEVEL STUDENTS.**

**A. HISTORY**

**1.** Major issues in Africa History-ICD
**2.** Major Events in Africa History-Mwaijage
**3.** The Political Economy, Imperialism-by Nabudere
**4.** Africa since 1800-4th edition-by Roland Oliver and Atmore
**5.** The making of modern Africa Vol .1
**6.** How Europe underdeveloped Africa-W.Rodney
**7.** The 20th century –by Duff.M.N
**8.** Europe from 1815 –by Peacock

**B. GEOGRAPHY**

**1.** Certificate Geography (Oxford) Form 3-by Mary Mugo , Robert Karuggah and Paul Kibuuka.
**2.** General Geography in diagrams –by R.B.Bunnet
**3.** Regional Geography-by Nyambali/Nyangwine
**4.** Photography Interpretation and Elementary Surveying for Secondary Level New Edition-by
S.E.Dura
**5.** Certificate Human and Economics Geography-by Morgan and Leong Chang

**C.KISWAHILI**

**USHAIRI**

**1.** Kimbunga-G.Gora (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili –TUKI) 1994
**2.** Chungu Tamu-T.A.Mvungi. (Tanzania Publisher House) 1985
**3.** Mapenzi Bora-S.Robert (Mkuki na Nyota) 2003
**4.** Fungate ya Uhuru-M.S. Khatibu (Macmillan and Aidan)

**RIWAYA**

**1.** Vuta n'Kuvute-Shafi .A.Shafi (Mkuki na Nyota)1999
**2.** Kufikirika –S.Robert (Mkukin a Nyota) 2003
**3.** Mfadhili –Hussein Tuwa (Mathew B/W and Stationery) 2007
**4.** Usiku utakapokwisha-Mbunda Msokile (Macmillan and Aidan) 2007

**TAMTHILIYA**

**1.** Morani-E.Mbogo (DUP)
**2.** Kivuli kinaishi-Said Mohamed (Oxford University Press)2007
**3.** Kwenye Ukingo wa Thim-E.Hussein (University Press)
**4.** Nguzoya Mama-DUP (1982)

**D. GENERAL STUDIES**

1. General Studies (Communication Skills for A-Level –M. Kadeghe)
2. General Studies notes (for A-Level Fir V & VI) G. Mshiu and N. Nyagwine

**E. ENGLISH LANGUAGE**

1. A Complete course for Form V & VI –Michael Kadeghe
2. English for Form V &VI – by Michael Kadeghe
3. Teaching English as a Foreign Language – G. Broughton et. Al
4. A grammar of Contemporary English – Quirk, et. Al
5. Longman English Grammar- L. G Alexander
6. The real English textbook for Advanced Level- by M. Kadeghe
7. Advance English Dictionary

**PART II**

**A. NOVEL**

1. The Beautiful One Are Not Yet Born- A. K Amah
2. A Man of the People – C. Achebe
3. Divine providence-Mkuki na Nyota
4. Encounters from Africa – Macmillan
5. The Rape of the Peal-Macmillan

**B. PLAYS/ DRAMA**

1. An Enemy of the People – H. Ibsen
2. I will marry when I want- EAEP
3. Rwanda Magere- by Okot Omtatah (1991)- Heinemann,Kenya
4. The Bride – EAEP
5. Black Mamba – EAEP

**C. POETRY**

1. Selected Poem from institute of Education
2. The Wonderful Surgeon and other Poem – Mkuki na Nyota